

***SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA GATITU
MTIHANI WA MWISHO WA MHULA WA KWANZA (2015)
KIDATO CHA NNE {FASIHI}***

JINA.....DARASA.....NAMB.....

MAAGIZO:Jibu maswali manne pekee.Swali la kwanza ni la lazima .Chagua mengine kutoka sehemu nyingine:

SEHEMU YA A: USHAIRI

Akili zangu
Zasimama ufuoni
Macho yake
Yakikagua bahari

Papa,mkali kama mauti
Anahangaisha samaki
Kwa ndaro na maringo
Daima akijigamba
Kwamba baharini
Haupo uwezo unaotisha
Wala tisho linalomweza
Wakati anaedelea kutiririka
Huku miongoni mwa samaki
Wingu zitohuzuni
Lazidi uzani

Kama kwa sumaku
Samaki wanavutwa pamoja
Na nyuma yangaoya umoja
Wanaenda mwendo wa mbele
Wakiimba nyimbo zenyе cheche

Kwa hasira zenyе moto
Papa anaongeza ukali
Bali umati wa samaki
Haulegei muumano
Wala mwendo wa mbele
Kupungua kasi

Mashambulizi makali
Ewaa! Mashambulizi!
Kutoka pande milioni
Dhidi ya papa muuaji

Sasa baharini
Nyimbo za ufanisi
Zinapaa angani

Kama moshi wa uhai
Na kubusu masikio
Kama muziki wa nyonza.

Maswali

- (a) Kwa kutoa mifano fafanua sifa zinazoufanya utungo huu kuwa shairi (alama 4)
- (b) Eleza mawazo ya mshairi katika shairi hili (alama 5)
- (c) Taja na ueleze mbinu tatu za lugha katika shairi hili (alama 6)
- (d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na shairi (alama 3)
- (i) Ndaro
- (ii) Cheche
- (iii) Nyonza

SEHEMU B: RIWAYA :Kidagaa Kimemwozea - Ken Walibora

“Asasi ya ndoa katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* inakabiliwa na changamoto nyingi.” Jadili.
(alama 20)

SEHEMU YA C : TAMTHILIA: Mstahiki Meya - Timothy M. Arege

“Wakisubiri ugonjwa nao utasubiri

a)Eleza muktadhawa dondo hili (Alama 4)

b)Taja na utolee mifano tamathali za usemi zozote **mbili** zilizotumika katika dondo (alama 4)

c)Jadili mbinu zozote **sita** alizozitumia Mstahiki Meya kuuendeleza utawala wake wa kidhalimu.
(alama 12)

SEHEMU YA D :HADITHI FUPI :DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

Kwa kurejelea hadithi **tano** za mwanzo katika diwani ya **Damu nyeusi**, eleza jinsi uozo katika jamii ulivuosawiriwa.
(Alama 20)

SEHEMU YA E:FASIHI SIMULIZI

- I.Fafanua sifa **tano** za ushairi simulizi. (Alama 10)
- II.Fafanua sifa na umuhimu wa malumbano ya utani katika jamii. (Alama 10)